# WAKRISTO: MABALOZI
## WA UFALME WA MUNGU

*Maagizo kuhusu Kuishi kama Mkristo.*



*Ukumbi wa Chuo cha Ambassador*

BOB THIEL, PH.D

# Wakristo:Mabalozi wa Ufalme wa Mungu

Maagizo Kuhusu Kuishi kama Mkristo.

**Bob Thiel, Shahada ya Uzamili.**

Copyright © 2018 by the *Nazarene Books*. ISBN 978-1-64106-025-7. Booklet produced by the *Continuing* Church of God and Successor, a corporation sole.1036 W. Grande Avenue, Grover Beach, California, 93433 USA.

*Jalada la Mbele: Picha ya Chuo cha Ukumbi wa Mabalozi na Joyce Thiel. Bob na Joyce walikuwa wakishiriki katika huduma za kanisa hapo wakipokea maagizo kuhusu maisha ya Mkristo, unabii, kazi ya Mungu, pamoja na kuwa mabalozi wa Kristo.*

# YALIYOMO


1. Wakristo wanapaswa kuwa
   Mabalozi wa Ufalme wa Mungu — Uk. 3

2. Je, ni jinsi gani Wakristo
   Wanapaswa Kuishi? — Uk. 7

3. Kuwa Mkristo Kunaathiri Maisha
   Yako Yote — Uk. 35

4. Uwezekano Wetu ni Mkubwa Mno
   kwa Sababu Mungu yuko
   Upande Wetu. — Uk. 55

5. Wakristo Wanakutana na
   Kuundeleza Ufalme wa Mungu — Uk. 62

Maelezo ya Mawasiliano — Uk. 69

# 1. Wakristo Wanapaswa Kuwa Mabalozi wa Ufalme wa Mungu

Ulimwengu na vyombo vyake vya habari una mitzamo tofauti kuhusu Ukristo na jinsi Wakristo wanapaswa kuishi.

Lakini mitazamo mingi hiyo HAINA msingi kwa Biblia au vitendo vya Wakristo wa kweli.

Je, Wajua jinsi Wakristo wanapaswa kuishi?

Je, historia ya Wakristo wa awali inaweza kutupatia vidokezo?

Je, Waweza kukubali amri na maagizo?

Kitabu hiki kimejaa na Maandiko ili kwamba mtu wa kweli aweze kujifundisha kuhusu vile Mungu yuataka watu wake waishi. Njia iliyotofauti sana ambayo Wakristo wengi wanaojidai kuwa Wakristo wanavyoishi.

**Mabalozi wa Kristo**

Mtume Paulo alifundisha kwamba Wakristo wanapaswa kuwa mabalozi wa ufalme wa Mungu unaokuja:

> 20 Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo… (2 Wakorintho 5:20).

> 17 Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu.
> 18 Mkiomba kwa Roho siku zote na maombi, mkikesha kila wakati mkiwaombea watakatifu wote.
> 19 Niombeeni na mimi pia, ili kila nifunguapo kinywa changu, nipewe maneno ya kusema, niweze kutangaza siri ya Injili kwa ujasiri,
> 20 ambayo mimi ni balozi wake katika vifungo. Ombeni ili nipate kuhubiri kwa ujasiri kama inipasavyo. (Waefeso 6:17-20)

Ni nini maana ya balozi? Kamusi ya *Merriam Webster* inatoa maelezo:

1: mjumbe wa kirasmi; hasa: wakala wa kidiplomasia wa cheo kikuu mwenye kibali kwa serikali ya kigeni au mtawala kama mwakilishi wa serikali yake ama mwenye uhuru ama amechaguliwa kwa uteuzi wa kidiplomasia wa kipekee na mara nyingi wa muda.

2: mwakilishi aliyeidhinishwa au mjumbe.

Lakini kama Wakristo, sisi sio wa muda lakini sisi ni wawakilishi wanaodumu wa Mungu, wa serikali yake na Ufalme wake.

Ijapokuwa Mtume Paulo alikuwa Myahudi na mwananchi wa Rumi (Matendo 21:39; 22:3, 28), aliandika kwamba uwenyeji wa Wakristo uko mbinguni:

> [20] Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia  Mwokozi, Bwana Yesu Kristo, (Wafilipi 3:20).

Mtume Paulo, hata kama hakulitumia neno balozi, anaunga mkono kauli hii akitiwa msukumo kuandika yafuatayo:

> [9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;[10] ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu, mliokuwa humkupata rehema, Bali sasa mmepata rehema. (1 Petro 2:9-10)

Wakristo wako katika sehemu ya ukuhani wa kifalme na taifa takatifu. Ni watu ambao hawatambuliki, kama vile mataifa mengine, lakini sasa ni mabalozi wa Ufalme wa Mungu unaokuja.

Je, umewahi kuyatambua hayo kuhusu Ukristo?

Kuhusiana na hayo, hayati Daktari Herman Hoeh alindika yafuatayo:

**Kanisa katika Unabii**

> Wakati watu wengi leo hii wanadhani kwamba KANISA la

kweli lingekua haraka liwe KUBWA, na kuwa shirika lenye nguvu, na kujitahidi kuwa na ushawishi katika ulimwengu, likifanya ulimwengu huu kuwa mzuri, likiwa na ushawishi wa kuimarisha ustaarabu wa ulimwengu, hakika ni kwamba Kristo hakulianza kanisa lake kwa kusudi hilo! Katika maombi yake ya mwisho kwa Kanisa lake MOJA, Yesu aliomba: ''Mimi nawaombea hao; siuombei ulimwengu… Baba mtakatifu, kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo… Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao sio wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao sio wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.'' (Yohana 17:9-16).

Wale walio wa Kanisa lake wametajwa kuwa ni wageni na wasafiri katika ulimwengu huu-yaani MABALOZI wa Kristo-mabalozi wanaowakilisha Ufalme WAKE ambao ni mgeni kwa ulimwengu huu-ijapokuwa ufalme huo sio wa ulimwengu huu! (Hoeh H. Why So Many Denominations? Tomorrow's World, April 1972).

Wakristo wanaishi katika dunia hii kama wawakilishi wa ufalme, wakitii mamlaka ya serikali ya dunia. Wakati kuna mgogoro katika kuzitii amri kuu za Mungu, Wakristo wanaendelea kumtii Mungu (Matendo 5:29), na hata wakati mwingine wanateseka kwa kuzitii amri hizo (1 Petro 4:15-16), lakini hawashiriki katika siasa zake.

Hata hivyo, mabalozi hawapaswi kuogopa hata kama wanatoka katika nchi ndogo yenye watu wachache. Kumbuka vile Yesu alivyowaambia watu wake:

32 Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. (Luka 12:32)

Wakristo wa kweli ni sehemu ya ''kundi dogo'', kama vile Mtume Paulo pia alisema kwamba kuna mabaki ambao wanachaguliwa kwa wakati huu wa sasa:

> [5] Basi ni vivi hivi wakati huu wa sasa, yako mabaki waliochaguliwa kwa neema. (Warumi 11:5)

Ukristo wa ukweli umenenwa vibaya kuanzia mwanzo. Wakati alifika Rumi, paulo aliambiwa:

> [22] …kwa maana katika habari za madhehebu hiyo imejulikana kwetu kwamba inanenwa vibaya kila mahali. (Matendo 28:22)

Sio ajabu kwamba wale wanaoshika Ukristo wa awali wananenwa vibaya siku hizi kila mara-na hata wale ambao ni washitaki wa ndugu zetu (Ufunuo 12:10) wanaowashitaki kwa mtandao wa intaneti.

Watu wa Mungu pia wanapaswa kuwa wajasiri:

> [7] Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.[8] Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, nawachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili. (Ufunuo 21:7-8)

Watu wasioamini ni waoga. Wakristo wanapaswa kusimama kwa ukweli (Mathayo 10:32-33).

## 2. Je, ni Jinsi Gani Wakristo Wanapaswa Kuishi?

Ikiwa Mungu amekuita uwe Mkristo, ni jinsi gani unapaswa kuishi? (Ikiwa unashangaa kuhusu wito wako tazama kijitabu chetu *Je Mungu Anakuita*?)

Wanakristo wanapaswa kuishije? Yaani Wakristo wa kweli.

Mada hii ni ngumu na pengine inachukuwa muda mwingi katika maisha ya binadamu ili aweze kuelewa, lakini kijitabu hiki kitajaribu kuwakilisha mengi, na hata ikiwezekana hoja zote kamili za jinsi twapaswa kuishi na pia hoja chache kuhusu kwa nini tunaishi.

Kama vile Paulo alivyoandika, tunapaswa kuishi kama vile mabalozi wa Yesu Kristo wanavyoishi.

Pia aliandika kwamba tunapaswa kumuiga kama vile alivyomuiga Kristo:

> 1 Niigeni mimi, kama nami ninavyomwiga Kristo. (1 Wakorintho 11:1) (NBT)

Wakristo wanapaswa waishi kama vile Yesu alivyoishi (Yohana 13:15;1 Wakorintho 11:1;1 Yohana 2:6) na kukubali yote aliyoamuru (Mathayo 28:18-20).

Yesu aliwahimiza watu kuishi kwa njia yake:

> 28 Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. 29 Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; 30 kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi. (Mathayo 11:20-30)

Pia aliyafundisha maonyo kwamba kutakuweko na taabu, lakini ataleta amani:

> [33] Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. (Yohana 16:33)

Katika Agano Jipya, Wakristo walichukuliwa kuwa tofauti sana na ulimwengu walimoishi kiasi kwamba jinsi walivyoishi ilijulikana kama ''Njia'' (Matendo 9:2;24:14,22) na hivyo ndivyo wanavyoita kwa kejeli faraka (Matendo 24:14) ama dhehebu (Matendo 24:14, NLT).

Ulimwengu huu unaishi kwenye ubinafsi, chini ya ushawishi wa Shetani, kwa kile kinachoitwa ''Njia ya Kaini'' (Yuda 11).

Wakristo ni mabalozi wa Ufalme wa Mungu na tunapaswa kuyaweka matumaini yetu kwa vitu vya kiroho si vitu vya kimwili hata kama tunaishi katika ulimwengu wa kimwili (Warumi 8:5-8). Kumbuka yafuatayo:

> [1] Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hiyo ulimwengu hautumtambui, kwa sababu haukumtambua yeye.[2] Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.[3] Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu. (1 Yohana 3:1-3)

Wakristo ni wana wa Mungu na tunaweka tumaini letu kwa Yesu-ulimwengu hawaweki matumaini yao kwa Mwokozi wetu.

Kwenye sala yake ya mwisho kwa ajili ya Kanisa la Kweli, Yesu aliomba:

> [12] Nilipokuwapo pamoja nao, mimi naliwalinda kwa jina lako ulilonipa, nikawatunza; wala hapana mmojawapo wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu, ili andiko litimie.[13] Na sasa naja kwako, na maneno haya nayasema

ulimwenguni, ili wawe na furaha yangu imetimizwa ndani yao.[14] Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.[15] Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu.[16] Wao sio wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. (Yohana 17:12-16)

Wale walio wa Kanisa lake wanajulikana kama wageni na wasafiri juu ya nchi-MABALOZI wa Kristo-wajumbe ambao wanawakilisha Ufalme wake ambao ni mgeni kwa ulimwengu huu-ijapokuwa sio wa ulimwengu huu! Twapaswa kutengwa na ulimwengu kwa ufuasi na kulitii neno la Mungu. Hayo yanatufanya kuwa tofauti na ulimwengu-pamoja na wengi wanaojidai kutumia Maandiko, lakini hawaishi kwa hayo maandiko.

Agano Jipya linaonyesha kwamba watu wa Mungu katika Agano la Kale:

> [13] …. Walikiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi. (Waebrania 11:13)

Mtume Paulo pia aliwaita Wakristo wageni na wasafiri:

> [1] Petro, mtume wa Yesu Kristo, kwa wateule wa Utawanyiko, wakaao hali ya ugeni katika Ponto, na Galatia, na Kapodokia, na Asia, na Bithinia;[2] kama vile Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mkapata kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo. (1 Petro 1:1-2)
>
> [11] Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho.[12] Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa. (1 Petro 2:11-12)

Polycarp wa Smirna, alipata kuteuliwa Askofu/Mchungaji/ Mwangalizi na Mitume, na alianza barua yake kwa Wafilipi kwa maneno yake yafuatayo:

> Polycarp na wazee wa Kanisa wakiwa pamoja naye, kwa Kanisa la Mungu walio wageni katika Filipi (Barua ya Polycarp kwa Wafilipi)

Kwa hivyo aliandika kwamba Wakristo katika Kanisa la Mungu walikuwa wakiishi kama wageni kule Filipi. Wazo kwamba Wakristo walikuwa wageni na wasafiri alilishika bado.

Mtume Paulo alizidi kuwaandikia Wakristo yafuatayo:

> [1] Basi, wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote.[2] Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasioghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu; [3]ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili. (1 Petro 2:1-3)

Wakristo wanahitaji maziwa safi ya neno, lakini wengi wanaokiri kuwa Wakristo hawajui zaidi maana ya maziwa hayo. Wengi wanaojidai kuwa Wakristo hawawezi kuishi kama wageni na wasafiri katika ulimwengu na pia kama mabalozi wa Yesu.

**Mkristo Halisi ni Nani?**

Wakristo halisi ni wale walio na Roho wa Mungu, wanaamini Biblia, wanajaribu kuenenda kama vile Yesu alivyoenenda, wanatunza amri, na pia wanaelewa upendo na kutenda.

Wakristo wa kweli wana Roho Mtakatifu wa Mungu:

> [9] Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamfuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.[10] Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu i hai, kwa sababu ya

> haki.[11] Lakini, ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho yake anayekaa ndani yenu. (Warumi 8:9-11)

Bila Roho wa Mungu huwezi kuwa Mkristo halisi. Yafuatayo ni yale Mtume Paulo aliyafundisha kuhusu kupewa Roho Mtakatifu:

> [38] Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.[39] Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. (Matendo 2:38-39)

Wakristo halisi wanasikia ujumbe wa injili, na kukubali kwamba wametenda dhambi na wanahitaji Mungu, wametubu dhambi zao (yaani uasi wa amri - 1 Yohana 3:4, kJV), na kukubali wito wa Mungu, Wanatangaza na kuamini kwamba Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi, kubatizwa kwa njia inayofaa, na kuwa na Roho Mtakatifu (Matendo 2:39; warumi 8:9-11).

Kupokea kwa Roho Mtakatifu kunafanya Mkristo wa kweli kuwa ''hekalu la Mungu'' (1 Wakorintho 3:16-17) na Wakristo wanapaswa kuishi kwa njia inayofaa.

Mungu anajua walio wake:

> [9] Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu (Wagalatia 4:9)

> [3] Lakini mtu akimpenda Mungu, huyo amejulikana naye (1 Wakorintho 8:3)

> [11] …lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu (2 Wakorintho 5:11)

[77] Uwajulishe watu wake wokovu, katika kusamehewa dhambi zao.

Kwa hivyo, Mungu mwenyewe anawajua Wakristo wa kweli.

Wakristo wa kweli wanashika amri na kujaribu kuenenda vile Yesu Kristo alivyoenenda:

> [4] Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.[5] Lakini alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Na hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.[6] Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda. (1 Yohana 2:4-6).
>
> [16] Nchi ikamsaidia mwanamke…[17] ... akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu (Ufunuo 12:16-17).
>
> [12] Hapa ndipo subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu. (Ufunuo 14:12).

Wengi ambao wanakiri kuwa Wakristo wamechagua kuenenda tofauti na vile Yesu alivyoenenda. Biblia na rekodi nyingine za historia ya kanisa zinaonyesha kwamba Wakristo wanapaswa kujitahidi kushika amri kumi za Mungu (tazama pia kitabu chetu cha mtandao *Amri Kumi: Torati, Ukristo, na Mnyama na Historia inayoendelea ya Kanisa la Mungu*).

Yesu pia alifundisha:

> [35] Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi. (Yohana 13:35)
>
> Madhehebu mengi ambayo wanakiri kuwa Yesu ni Kristo, hata hivyo, wanaruhusu vita na matendo mengine

ambayo hayaonyeshi upendo kati ya majirani.

Kama mabalozi, Wakristo hawashiriki katika jeshi, majaji ya kawaida, na hata hatupigi kura katika siasa za ulimwengu.

Mtume Paulo alifundisha:

> [12]Lakini zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kinginecho chote; bali ndiyo yenu iwe ndiyo, na siyo yenu iwe siyo, msije mkaangukia hukumu. (Yakobo 5:12)

Yesu alifundisha hayo pia katika mahubiri ya Mlima. Kwa hivyo, Wakristo wa kweli hawaapi.

Maisha yanahusu upendo siyo vita.

Wakristo wanafahamu mafundisho ya kimsingi ya kanisa kama vile yalivyoandikwa katika Waebrania 6:

> [1] Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu, tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, [2] na ya mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele. (Waebrania 6:1-2).

Na pia Wakristo wanatembea kwa Njia ile ambayo Mitume walitembea na kuinena.

**Wakristo Wanapitia Magumu**

Kumbuka yale ambayo nabii Yeremia aliambiwa kurekodi:

> [11] Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.[12] Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza.[13] Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.[14] Nami nitaonekana kwenu, asema BWANA,

name nitawarudisha watu wenu waliofungwa, nami nitawakusanya ninyi, nikiwatoa katika mataifa yote, nakatika mahali pote, nilikowafukuza, asema BWANA; nami nitawaleta tena, hata mahali ambapo kutoka hapo naliwafanya mchukuliwe mateka. (Yeremia 29:11-14).

Kumbuka kwamba mpango ulikuwa ni kufanywa mateka. Kuwa msafiri, mgeni na balozi. Huo bado ndio mpango kwa Wakristo walioko kwa wakati huu.

Yeremia pia alirekodi:

> 28 ambaye ametuma watu kwetu katika Babeli, kusema, Uhamisho huu ni wa siku nyingi; jengeni nyumba, mkakae ndani yake; pandeni bustani, mkale matunda yake. (Yeremia 29:28).

Kumbuka kwamba wale waliofanywa mateka wangepanda na kujenga na kupata matunda. Kupanda kunahitaji imani. Kutafsiri Makala katika lugha mbalimbali, pamoja na zile lugha ambazo hazina washiriki kunahitaji I mani-lakini hiyo ndiyo sehemu ya kazi ambayo sisi katika Kanisa la Mungu *Linaloendelea* twafanya. Na kama vile mateka, twapaswa kuzaa matunda.

Kwa kuishi, kupenda na kuzaa matunda kama vile Yesu alivyofundisha, Wakristo watachukiwa na kuteswa:

> 16 Si ninyi mlionichagua mimi, Bali ni mimi niliyewachagua, nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni. 17 Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana. 18 Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. 19 Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. 20

Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu.[21] Lakini haya yote watawatenda kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyenipeleka.[22] Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao.[23] Yeye anichukiaye mimi humchukia na Baba yangu.[24] Kama nisingalitenda kwao kazi asizozitenda mtu mwingine, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa wametuona mimi na Baba yangu na kutuchukia.[25] Lakini litimie lile neno lililoandikwa katika torati yao, Walinichukia bure. (Yohana 15:16-15)

[22] …imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. (Matendo 14:22)

Siyo kwamba taabu zote zitatoka kwa ulimwengu 'mpana.' Familia na marafiki pia wanaweza kusababisha taabu. Kumbuka kwamba Yesu alifundisha kuhusu masuala ya familia, akifuatwa na Mtume Petro:

[35] Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu;[36] na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake.[37] Apendaye baba au mama kuliko mimi, hastahili; wala mwana au binti kuliko mimi; hastahili.[38] Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili.[39] Mwenye kuiona nafsi yake ataipotea, naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona. (Mathayo 10:35-39)

[4] mambo ambayo wao huona kuwa ni ajabu ya ninyi kutokwenda mbio pamoja nao katika ufisadi ule ule usio na kiasi, wakiwatukana. (1 Petro 4:4)

Hiyo haimanishi kwamba ukose heshima kwa wazazi wako (Mathayo 15:4-6) ama kuleta kisirani-tunaswa ''kukaa katika

amani na watu wote'' (Warumi 12:18). Yesu na Mtume Petro hasa wanasema kwamba wale walioitwa wanaweza kuwa na matatizo na familia na hata marafiki. Kumbuka pia jambo fulani kutoka kwa Yesu na Petro, likifuatwa na jambo lingine kutoka kwa Mtume Paulo:

> 16 Angalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua. 17 Jihadharini na wanadamu; kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga. (Mathayo 10:16-17)

> 15 Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu. 16 Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayn arishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo. 17 Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya. (1 Petro 3:15-17)

> 15 Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. 16 Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu. (2 Timotheo 2:15-16)

Wakati unawasiliana na wale ambao hawamo kanisani, na hata pia wale waliomo kanisani, Wakristo wanapaswa kuwa na hekima ili wasiwaharibu. Na pia Wakristo wanapaswa kusoma ili wapate kuyajibu maswali ambayo wengine wanaweza kuyauliza. Siyo kwamba tujaribu kulazimisha dini yetu kwa koo za wengine, lakini tujaribu kujibu kwa unyenyekevu wale ambao wanamaanisha. Hata hivyo tunapaswa kuepukana na maneno yasiyo na maana (Mathayo 7:6; 1 Timotheo 1:4)

Yesu pia alionya:

[33] Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. (Yohana 16:33)

Na kufanya yale ambayo tunapaswa kufanya kama Wakristo inaonyesha kwamba tuna imani. Na siyo rahisi kufanya vile inavyotakikana.

[22]…Mwamini Mungu (Marko 11:22)

Kulikuweko na wazushi katika nyakati za mitume ambao hawakuamini kwamba wanaweza kutenda jambo lolote na walidhani kwamba imani yao ilitosha. Lakini kumbuka vile Yakobo alivyowaambia:

[22] Lakini iweni watendaji wa neno, Wala si wasikiaji tu, hali mkidanganya nafsi zenu.[23] Kwa sababu mtu akiwa msikiaji tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalii uso wake katika kioo.[24] Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.[25] Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. (Yakobo 1:22-25)

[14] Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile Imani yaweza kumwokoa? [15] Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki,[16] na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?[17] Vivyo hivyo na imani, isipokuwa na matendo, imekufa nafsini mwake.[18] Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.[19] Wewe waamini kwamba Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani

> nao waamini na kutetemeka.[20] Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai? (Yakobo 2:14-20)

Pengine kwa maneno haya ndiyo maana Martin Luther alipinga sana kitabu hiki cha Yakobo.

**Kwa hivyo, ni jinsi gani Mkristo anapaswa kuishi?**

Tangia awali katika historia nzima, Wakristo wa kweli wamekuwepo, kama vile Kristo alivyotabiri (Mathayo 16:18; Ufunuo 2 na 3).

Wamekuwa mbali sana na maabishano ya uongo wa siri ya uasi (2 Wathesalonike 2:7), lakini wamejaribu kutunza amri.

Wakristo halisi wanaishi tofauti sana na wale wanaokiri kuwa Wakristo na mara nyingi walikuwa wakiteswa kwa sababu hiyo.

Wakristo halisi wanaelewa Mahubiri yaliyohubiriwa na Yesu juu ya Mlima:

> [1] Naye alipowaona makutano, alipanda mlimani; na alipokwisha kuketi, wanafunzi wake walimjia;[2] akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema, [3] Heri walio, maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao.[4] Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika.[5] Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi.[6] Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.[7] Heri wenye rehema; Maana hao watapata rehema.[8] Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu.[9] Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu.[10] Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao.[11] Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu.[12] Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.[13] Ninyi ni

chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.[14] Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.[15] Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.[16] Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu. wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.[17] Msidhani kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza.[18] Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka hata yote yatimie.[19] Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.[20] Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.[21] Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu.[22] Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto.[23] Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako,[24] iache sadaka yako mbele ya madhabahu,  uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.[25] Patana na mshitaki wako upesi, wakati uwapo pamoja naye njiani; yule mshitaki asije akakupeleka kwa kadhi, na kadhi akakupeleka kwa askari, ukatupwa gerezani.[26] Amin, nakuambia, Hutoki humo kamwe hata uishe kulipa senti ya mwisho.[27] Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini;[28]

lakini mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke
kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni
mwake.[29] Jicho lako la kuume likikukoshesha, ling'oe
ulitupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako
kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika
jehanum.[30] Na mkono wako wa kuume ukikosesha, ukate
uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako
kimoja wala mwili wako mzima usitupwe katika
jehanum.[31] Imenenwa pia, Mtu akimwacha mkewe, na
ampe hati ya talaka;[32] lakini mimi nawaambia, Kila mtu
amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati,
amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa,
azini.[33] Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa,
Usiape uongo, ila, mtimizie Bwana nyapo zako;[34] lakini
mimi nawaambia, Usiape kabisa; hata kwa mbingu; kwa
maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu;[35] wala kwa nchi
kwa maana ndiyo pa kuwekea miguu yake; wala kwa
Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa Mfalme mkuu.[36]
Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya
unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.[37] Bali
maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo; kwa kuwa
yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu.[38] Mmesikia
kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino.[39]
Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu;
lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili.[40]
Na mtu atakaye kukusitaki na kuitwaa kanzu yako,
mwachie na joho pia.[41] Na mtu atakayekulazimisha
mwendo wa maili moja, nenda naye mbili.[42] Akuombaye,
mpe; naye atakayekukopa kwako, usimpe kisogo.[43]
Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na,
umchukie adui yako;[44] lakini mimi nawaambia,
Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,[45] ili
mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana
yeye huwaangazia jua lake waovu na wema,

huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.[46] Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watosha ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? [47] Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo? [48] Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. (Mathayo 5:1-48)

[1] Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni.[2] Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu.[3] Amin, nawaambieni, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume;[4] sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. (Mathayo 6:1-4)

Mambo haya yanawakumba Wakristo kwa kazi zao, shuleni, nyumbani na wakati wote. Wao sio Wakristo tu wakihudhuria huduma za kanisa. Wanajaribu ili wasiishi kama wanafiki. Na pia hawaangalii video za ngono, hawashiriki katika uzinzi na ushoga, ama kuishi maisha ya chuki. Tunapaswa kujaribu kuwa wakamilifu ili kwamba tuwe wana wana na binti za Mungu. Tuna nafasi nzuri sana kama Wakristo.

Wakristo wa kweli wana vipao mbele halisi na wanatafuta Ufalme wa Mungu.

[25] Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, namwili zaidi ya mavazi? [26] Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu

wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao?
[27] Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongezea
kimo chake hata mkono mmoja? [28] Na mavazi, ya nini
kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi
yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti[29] nami
nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake
yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya hayo.[30] Basi,
kama Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo
leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana
kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? [31] Msisumbukie,
basi, mkisema Tule nini? Au Tunywe nini? Au tuvae nini?
[32] Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu
Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo
yote.[33] Bali utafuteni, kwanza ufalme wake, na haki yake;
na hayo yote mtazidishiwa.[34] Basi msisumbukie ya kesho;
kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa
siku maovu yake. (Mathayo 6:25-14)

Mabolozi wanafanyia serikali yao kazi kila wakati. Wakristo wanapaswa kufanya kazi katika serikali ya Mungu na ufalme wake unaokuja.

Kuutafuta ufalme wa Mungu inamaanisha kwamba Wakristo halisi hawalegezi amri za Mungu kwa sababu ya biashara, familia, tamaa, ama kwa makusudi mengine (pia tazama kijitabu kiitwacho *Injili ya Ufalme wa Mungu na Amri Kumi, Torati, Ukristo, na Mnyama*).

Kumbuka kwamba Mtume Paulo aliandika:

[14] Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo
sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na
uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? [15] Tena
pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye
aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini? [16]
Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na

sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.[17] Kwa hiyo Tokeni kati yao, Mkatengwe nao asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.[18] Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi. (2 Wakorintho 6:14-18)

Wakristo halisi hawafai kuwaoa Wakristo wasio halisi-ina maana kwamba wapate tu kuwaoa Wakristo wa Kanisa la Mungu la kweli. Uzoefu unaonyesha kwamba ukioa nje ya Kanisa mambo ya kiroho hayaendi vizuri.

Himizo la Paulo pia ni onyo dhidi ya aina tofauti ya biashara na mashirikiano mengine. Na pia ni onyo dhidi ya muungano usiofaa.

Wewe ni mtu wa kipekee. Uzoefu wa maisha yako, nk. unakufanya uwe mtu ambaye anaweza kuonyesha upendo kwa njia ya kipekee. Yesu ana mahali palipotengenezwa kwa ajili yako (Yohana 14:2-3). Lakini kama Mkristo, unazo karama sasa ambazo twahimidiwa:

[16] Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. (Mathayo 5:16)

[10] Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe. (Mhubiri 9:10)

[31] Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.[32] Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu.[33] vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika

> mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa. (1 Wakorintho 10:31-33)

Kama wanafiladelfia, hata kama tunapambana, unapaswa KUTOA, ili upate kugawa na kusaidia ulimwengu huu mbaya. Utakuwa na hamu ya kuweka moyo wako wote katika Kazi ya Mungu. Unapaswa kuwa na bidii kwa kujua ukweli (Yohana 17:17-19;1 Petro 3:15-16). Utakuwa na hamu ya kushiriki katika kuuonya ulimwengu kuhusu matukio ya kiajabu yatakayotokea kabla ya mwisho wa dahari. Utajua kwamba ulimwengu huu wa sasa hautaendelea jinsi ulivyo. Mungu anaweza akakutumia katika mateso ya mwisho kutoa ushuhuda wenye nguvu (Marko 13:9) ambao utasaidia ''kufundisha wengi'' (Danieli 11:32-33).

Kumbuka pia yafuatayo:

> 17 Mjumbe mbaya huanguka maovuni; Bali mjumbe mwaminifu ni afya. (Mithali 13:17)

Uwe mjumbe mwaminifu ili ushiriki katika njia ya mafundisho ya Mungu na ufalme wake unaokuja ukiyafundisha ulimwengu huu mbaya, ambao Ibilisi ameudanganya.

Kumbuka kwamba Wakristo wa kweli wanapaswa kuomba na Biblia inafundisha hivyo (Mathayo 6:5-7). Katika nyakati za kisasa tunashauriwa kwamba Wakristo wanapaswa kuomba dakika thelathini kwa siku, ilhali Biblia haijasisitiza sana kuhusu muda wa maombi ya kila siku. Hata hivyo, Biblia inasema kwamba ''tuombe bila kukoma'' (1 Wathesalonike 5:17), hii inaonyesha kwamba tuombe kila mara. Wakristo basi wanafaa kuomba (ukitaka kujua zaidi kuhusu maombi, tazama kijitabu chetu *Maombi: Biblia Inafundisha Nini?)*

Wakristo wanapaswa kutafakari juu ya amri za Mungu na njia zake (Zaburi 19:7). Ukweli ni kwamba Mungu ni upendo (1 Yohana 4:8,15) kwa hivyo HANA ubinafsi. Amri za Mungu

zaonyesha upendo kwa Mungu na kwa jirani (Marko 12:29-31; Yakobo 2:8-11). Njia za ulimwengu ni za ubinafsi na zinaelekea mautini (Warumi 8:6). Wakristo wanagundua kuwa kuzitunza sheria na amri za Mungu inaonyesha upendo na amri hizo si nzito:

> 5 Katika hili twajua kwamba twapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. 3 Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito. (1 Yohana 5:2-3)

Wakristo halisi wanasoma Biblia (kwa wale ambao wanaweza kusoma) na pia wanasoma kila siku (Matendo 17:11; Waefeso 6:17). Katika nyakati hizi za kisasa inapendekezwa kwamba Wakristo wanafaa kusoma dakika thelathini kila siku. Hata hivyo, Biblia haijasema chochote kuhusu kauli hiyo.

Agano Jipya lafundisha kwamba, ''Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote'' (Wagalatia 6:6). Wakristo wa kweli wanatoa zaka (Mathayo 23:23). Na zaka aina tofauti (Kumbukumbu 14:22-29). Zaka inafanyiwa hesabu kutoka kwa mapato. Katika mtazamo wangu, faida wavu hutolewa baada ya mtu kutoa ushuru kwa sababu Wakristo pia wanapaswa kutoa ushuru (Marko 12:14-17; Mathayo 17:24-27). Wakristo pia wanapaswa kutoa matoleo ya hiari, pamoja na ya Sikukuu (Kumb. 16:16-17;2 Wakorintho 9:6-15).

Watu ambao hawatoi sio Wakristo wa kweli. Kumbuka kwamba ''Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu'' (1 Wakorintho 9:7). KUMBUKA: Wacha niongeze kwamba mimi, Bob Thiel, SICHUKUI mshahara kutoka kwa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), kwa hivyo siandiki haya ili watu watoe alafu nichukue kutoka kwa matoleo au zaka hizo. Kutoa kinafaidi mtu kiroho, kwa hivyo ikiwa mtu hawezi kufanya hivyo, basi huyo haishi kama Mkristo wa kweli.

Yesu alikutana na tajiri aliyekuwa akijidai kuwa amejitolea kwa ajili ya Mungu, lakini kumbe alishikilia mali yake kuliko chochote (Mathayo 19:16-22). Lakini maskini na wale walio katika kiwango cha wastani pia wana shida kama hiyo. Wengi hawana imani ya kutosha:

> [9] Mheshimu BWANA kwa mali yako. Na kwa malimbuko ya mazao yako yote.[10] Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, Na mashinikizo yako yatafurika divai mpya. (Mithali 3:9-10)

> [27] Mwenye kuwagawia maskini hatahitaji kitu; Bali afichaye macho yake atakuwa na laana nyingi. (Mithali 28:27)

> [8] Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi, Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka kwa dhabihu.[9] Ninyi mmelaaniwa kwa laana, maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote.[10] Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. (Malaki 3:8-10)

> [6] Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote.[7] Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi, kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.[8] Maana yeye apnadaye kwa mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho atavuna uzima wa milele.[9] Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.[10] Kwa hiyo kadri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio. (Wagalatia 6:6-10)

Uwe na imani na utoe kama vile Mungu anawataka watu wake wafanye. Kumbuka:

> [20] Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona.[21] Na amri hii tumepewa nay eye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu ampende na ndugu yake. (1 Yohana 4:20-21)

Wanafiladelfia hawana chuki na ndugu zao. Wanaonyesha upendo kwa kutoa na kuwasaidia katika vitu vya mwili na kiroho. Wanapenda wengine pia kwa kusaidia kutimiliza Mathayo 24:14 na Mathayo 28:19-20.

Yesu alisema kwamba wanafunzi wake watafunga (Marko 2:20). Na hata kama wengi wanaoweza kufunga wanaweza kufunga katika siku ya Upatanisho kila mwaka, kihistoria Kanisa la Mungu lilipendekeza mara moja kila mwezi kama lengo zuri la kufunga- hata hivyo Biblia haijataja kwamba ni mara ngapi tunapaswa kufunga.

Wakristo wa ukweli hawaendi kuchanjiwa chale au alama katika miili yao (Walawi 19:28).

Wakristo wa kweli hawali aina za nyama zisizokubalika (Walawi 11:4-8,10-20,23-30; Kumbukumbu 14:3,7-8,10,12-19). Kwa sababu ya kauli hii, wengine wameuawa na Wagiriki-Rumi ambao wanajidai kuwa Wakristo.

Nikiongea juu ya vyakula, Mungu anawaambia watu wake ‘’mle kilicho mema’’ (Isaya 55:2), kwa hivyo Wakristo wanapaswa kumakinika kuhusu lishe yao ili kwamba wasile kisicho mema. Pia Wakristo wasivute sigara, viko, na hata bangi.

Wakristo wa kweli wasikose kuaminika mahali wanapofanyia kazi au shuleni. Hawadanganyi au kusema uongo. Hawafuati dhambi katika mashirika ya kufanyia kazi. Wakristo hawasomi nyota, kushiriki katika uchawi, ama hawaendi kwa waganga (Walawi 19:26; Kumbukumbu 18:10). Wacha niseme kwamba wakati wanajimu wengi na wale wanaofuata unajimu wanadai kuwa Wakristo, madai hayo siyo ukweli.

Wakristo wa kweli hawana sanamu nyumbani mwao ama hawabebi ''hirizi ya bahati,'' n. K.

''Maneno mabaya au matusi'' yasitoke kwa vinywa vya Wakristo wa kweli (Wakolosai 3:8; tazama pia kijitabu chetu katika mtandao *The Ten Commandments: The Decalogue, Christianity, and the Beast*).

Wakristo wa kweli wanaelewa umuhimu wa Amri za Mungu na kuwa watahukumiwa kwa matendo yao:

> 13 Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa: Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla, ndiyo impasayo mtu.14 Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kwa kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya. (Mhubiri 12:13-14)

Wakristo wanapaswa kuwafundisha na kuwalea watoto wao vizuri (1 Wathesalonike 2:11; Waefeso 6:1; 1 Timotheo 3:4,12;5:4,10,14; Tito 1:6;2:4).

Wanawake Wakristo hawapaswi kuwa na nywele fupi na wanaume pia kuwa nywele ndefu kama ya wanawake (1 Wakorintho 11:14-15). Kwa vile makuhani wa kipagani walikuwa wakinyoa denge pande za vichwani, hiyo haionyeshi matendo ya Waume Wakristo (Walawi 19:27;21:5).

Wakristo pia wasivae mavazi yasiyowapasa maumbile yao ((Kumbukumbu 22:5) na wavae kistaarabu na kwa heshima (1 Timotheo 2:9).

Wakristo wanapaswa kuhudumia watu bila madharau (1 Timotheo 4:12,5:1-2). Wale ambao hawajaoa pia wanaweza kusoma kitabu chetu kwa mtandao: Dating: *A Key to Success in Marriage, a practical dating guide for Christians,* ambacho kinapatikana katika tovuti ya www.ccog. Org. Pia tuna uhuishaji katika CCOG Animations katika chaneli ya YouTube: *First Date: Worldly vs. Christian*.)

Wakristo hawashiriki katika kulewa ama kushiriki katika uzushi usiofaa, kwa hivyo wanaweza kuwa watu wasio na umaarufu na wale waliokuwa marafiki zao wa awali kama vile Mtume Petro alivyoandika:

> 1 Basi kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili wake, ninyi nanyi jivikeni silaha ya nia ile ile; kwa maana yeye aliyeteswa katika mwili ameachana na dhambi. 2 Tangu sasa msiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu, Bali katika mapenzi ya Mungu, wakati wenu uliobaki wa kukaa hapa duniani. 3 Maana wakati wa maisha yetu uliopita watosha kwa kutenda katika ufisadi, natamaa, na ulevi, na karamu za ulafi, na vileo, na ibada ya sanamu isiyo halali; 4 mambo ambayo wao huona kuwa ni ajabu ya ninyi kutokwenda mbio pamoja nao katika ufisadi ule ule usio na kiasi, wakiwatukana. (1 Petro 4:1-4)

Kwa hivyo Wakristo wanatukanwa kwa sababu hawashiriki katika matendo ya ufisadi. Mtume Paulo pia aliandika:

> 12 Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. 13 Lakini kama

> mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.[14] Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia. (1 Petro 4:12-14)

Kwa hivyo Wakristo watarajie matukio mabaya kutoka kwa ulimwengu dhidi yao. Wakristo wa kweli wanagundua hayo lakini wanaendelea. Wanaelewa himizo la Yesu:

> [21] Na ndugu atamsaliti nduguye ili auawe, nababa atamsaliti mwana, na wana watawainukia wazazi wao, na kuwafisha.[22] Nanyi mtakuwa mkiichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka.[23] Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu.[24] Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake.[25] Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, namtumwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba Beelzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake? [26] Basi, msiwaogope, kwa maana hakuna neno lililositirika, ambalo halitajulikana. (Mathayo 10:21-26)

**Sherehe, Sikukuu na Sabato**

Je! Unapaswa kuadhimisha Sikukuu za Mungu au Sherehe za Kishetani?

Wengi ambao wanadai kuwa Wakristo wanaadhimisha sherehe za kishetani.

Ijapokuwa kama wale Wakristo wa awali, Wakristo Wanafiladelfia leo hii hawashiriki katika kuadhimisha sherehe za kipagani (tazama kitabu chetu katika mtandao *Should You Keep*

*God's Holy Days or Demonic Holidays?*) ama kwa kawaida (wengine hawawezi kujua kuhusu hizi) sherehe za kuzaliwa.

Hii inaweza kuwafanya wawe tofauti sana na majirani yao, wafanyikazi wenzao, waajiri wao na hata familia zao (Mathayo 10:34-39).

Wakristo wa kweli wanapaswa kuadhimisha Sikukuu za Mungu za Kibiblia.

Kumbuka jambo fulani ambalo Mtume Paulo aliandika:

> 18 Watoto, ni wakati wa mwisho; na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo. Kwa sababu hiyo twajua ya kuwa ni wakati wa mwisho. 19 Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu. (1 Yohana 2:18-19)

Mabadiliko ya kwanza ni kutofuata yale yaliyofuatwa na Mtume Yohana, kama vile wengine walibadilisha siku ya Pasaka kutoka tarehe 14 ya Nisan/Abibu hadi Jumapili yaani siku ya kwanza ya Juma. Hii ni pamoja na kuwa Mitume Yohana na Filipo waliadhimisha Pasaka tarehe 14 na hawakubadilisha siku kuwa Jumapili. (Hata Mtume Paulo alifanya vivyo hivyo-tazama kitabu chetu kwa mtandao wa intaneti: *Continuing History of the Church of God*).

Kuadhimisha siku ya 14 ya Pasaka kama Wakristo waaminifu kulisababisha vifo kama vile Mtawala wa Rumi Theodosia aliamuru katika mwisho wa karne ya nne.

Je, waweza kustahimili mateso ya maneno? Omba ili ustahimili (waweza pia kutazama kijitabu chetu katika mtandao wa intaneti

*Prayer: What Does the Bible Teach*?). Sababu ambayo tuna vitabu vyetu katika mtandao kama vile Is God's Existence Logical? na Proof Jesus is The Messiah (ni kwamba vitabu vyetu vyote ni vya bure kwa mtandao wa intaneti katika www.ccog.Org) ili kwamba upate kuujua thibitisho la ukweli (Luka 1:4) na pia uweze kustahimili mateso yanayokuja (Danieli 7:25,11:28-36).

Wakristo wa kweli wanajitayarisha kabla hawajala Pasaka kila mwaka kwa kujitathmini wenyewe (2 Wakorintho 13:5). Pia wanatoa vitu vya chachu vyote kutoka kwa nyumba zao na kuila mikate isiyochachwa kwa muda wa siku saba kila mwaka wakijaribu kujiepusha na kuila iliyochachwa kwa muda huo (tazama kijitabu chetu kwa mtandao *Should You Keep God's Holy Days or Demonic Holidays*?)

Wakristo wanaadhimisha Sikukuu ya Pentekoste na ya Baragumu.

Wakristo pia wanaadhimisha Siku ya Upatanisho (inayoitwa ''Kufunga'' katika Matendo 27:9) kwa wale wanaoweza kufunga kabisa siku hiyo kwa kutokula na kutokunywa maji (wale walio na shida ya kiafya, kina mama wanaonyonyesha, watoto wachanga, n. K hawafungi). Hii imekuwa ngumu sana kwa wengi kwa sababu wengine wanapata kuumwa na kichwa na wengine pia wana masuala mengine na kufunga. Kwa sababu ya shida nyingine, mimi nilikuwa karibu kuwekwa gerezani kwa sababu nilikosa kwenda kazini Siku ya Upatanisho (Nilikuwa nafanya katika Jeshi la Marekani wakati huo).

Wakristo wanaadhimisha Sikukuu ya Makambi ambao inabidi watu wasafiri kutoka maeneo yao wanakoishi. Katika Kitabu cha Zaburi inaitwa ''Sikukuu ya kusafiri'' (Zaburi 42:4). Aina hii ya kusafiri kunaweza kusababisha shida kwa wafanyikazi, wafanyibiashara, wanafunzi na wazazi.

Wakristo wanatunza Sabato kuanzia machweo ya Ijumaa hadi machweo ya Jumamosi kila juma.

> [3] Sasa sisi ambao tumeamini tunaingia katika ile raha, kama vile Mungu alivyosema, ''Hivyo natangaza kwa kiapo katika hasira yangu, ''Kamwe hawataingia rahani mwangu.'' Lakini kazi ile ilikamilika tangu kuumbwa kwa ulimwengu.[4] Kwa mahali fulani amezungumza kuhusu siku ya saba, akisema: ''Katika siku ya saba Mungu alipumzika katika kazi zake zote.'' [5] Tena hapo juu asema, '' Kamwe hawataingia rahani mwangu.'' [6] Kwa hiyo kwa kuwa inabaki kuwa wazi kwa ajili ya wengine kuingia, nao wale wa kwanza waliopokea Injili walishindwa kuingia kwa sababu ya kutokutii…[9] Kwa hiyo basi, imebaki raha ya Sabato kwa ajili ya watu wa Mungu,[10] kwa kuwa kila mmoja aingiaye katika raha ya Mungu pia hupumzika kutoka kazi zake mwenyewe, kama vile naye Mungu alivyopumzika kutoka kazi zake.[11] Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha hiyo, ili kwamba asiwepo ye yote atakayeanguka kwa kufuata mfano wao wa kutokutii. (Waebrania 4:3-6,9-11, NBT)

Wakristo wanapaswa kutii amri ya Sabato. Ndiyo, kutii Sabato imesababisha wengine wameachishwa kazi na wengine wamechukiwa na wafanyikazi wenzao. Kutunza Sabato pia inamaanisha kwamba hakuna kununua vitu siku hiyo. Kwa upande mwingine, nafahamu kwamba Biblia inaruhusu kukula hotelini ukisafiri ama kutumia pesa kwa hali ya dharura (kwa mfano kuenda hospitali), na pia kuna sababu nyingine za kidharura. Lakini kwa jamii nyingine huwezi kukosa kununua siku ya Jumamosi kwa sababu hawaruhusu kununua siku ya Jumapili katika maeneo mengi.

Amri ya nne ya Sabato pia ni pamoja na kwamba tufanye kazi, na Wakristo wanaelewa kwamba wanapaswa kufanya kazi ili

wapate kula (2 Wathesalonike 3:10-12) na wasijishughulike na mambo ya wengine (2 Wathesalonike 3:11). Ni vizuri ukiwa na zaidi ya kazi moja (Mhubiri 11:6).

Kwa vile machweo yanabadilika hasa katika maeneo yaliyo mbali na ikweta, wengine wetu wanapaswa kuraukia kazi mapema ya Ijumaa katika siku za majira ya baridi, Pia kutunza Sabato inamaanisha hakuna kushiriki katika shughuli za michezo katika siku ya Sabato. Lengo ni kuwa katika vitu vya Mungu na siyo kufanya raha zetu (Isaya 58:13-14).

Wakati mambo haya yanaonekana magumu na mengine ni magumu kuyaelewa (2 Petro 3:16), Wakristo wa ukweli wanakubali:

> 9 Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. (Isaya 55:9)

Wakristo wanafanya hivyo kwa sababu wana imani, siyo kwamba wana imani kwamba Mungu yupo peke yake lakini kwamba njia zake ni nzuri na zitakuwa na matokeo mema mwishowe:

> 6 Lakini pasipo Imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. (Waebrania 11:6)

Jambo hili linatofautisha Wakristo wa kweli na mapepo ambao wanaamini Mungu yupo na wengine pia ambao wanasema kwamba wameamini Mungu yupo (Yakobo 2:19), lakini hawawezi kuyaamini aliyoyafundisha.

Kuna njia mbili za maisha-ya Mungu na ya Shetani. Njia ya Mungu ni njia ya kutoa.

Kwa hivyo, tumeangalia ‘maziwa ya neno’ (1 Petro 2:2) kuhusu kuwa Mkristo wa kweli.

## 3. Kuwa Mkristo Inabadilisha Maisha Yako Yote

Unaweza kufikiri kwamba haya ni magumu sana. Lakini kuwa Mkristo inabadili maisha yangu yote.

Na Wakristo wa kweli wanapaswa kuwa dhabihu iliyo hai na wasifuatishe namna ya dunia hii:

> [1] Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.[2] Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. (Warumi 12:1-2)

Balozi wa kweli anaweza kutoa uhai wake kwa ajili ya serikali yake. Balozi wa kweli hawezi kuzifuatisha serikali za kigeni ambazo zinaenda kinyume na serikali yao. Wakristo wanapaswa kujitolea maisha yao kwa Mungu na wasifuatishe ulimwengu huu. Mtume Paulo anaiita kazi inayopendeza.

Mungu anataka kujitolea kamili. Hiyo inahitaji imani (tazama kijitabu chetu cha mtandao *Imani kwa Wale Walioitwa na Kuchaguliwa)*.

Mtume Paulo aliandika ''vaeni silaha zote za Mungu'' (Waefeso 6:11). Kumbuka pia alichofundisha:

> [20] Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. (Wagalatia 2:20)
>
> [17] Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani. (Warumi 1:17)

Kusulubishwa na Kristo kunaonyesha kujitoa kamili. Hii ni imani kamili. Hivyo ndivyo Wakristo wa kweli wanatofautiana na wengine wa kawaida.

Mtume Paulo pia aliandika:

> [28] Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. (Warumi 8:28)

Wakristo wana imani kwamba njia ambazo zimeandikwa kwa Biblia zitawafikisha kwa mema. Wengi wanaodai kuwa Wakristo hawana imani kwamba mambo yote yanafanyika vyema kwa wale wanaomwamini Mungu. Ikiwa unataka kujua kama Mungu anakuita, tazama kijitabu chetu kwa mtandao wa tovuti: *Is God Calling You*? Kinachopatikana katika [www.ccog. Org](http://www.ccog.org)

Kama Wakristo, tunavuka toka maziwa ya neno kuelekea chakula kamili:

> [2] Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi (1 Wakorintho 3:2)

Kinachofanya Biblia ifundishe kwamba batiso ni ya kujitumbukiza kwa maji mengi ni kusaidia kuoonyesha kwamba umejitoa kabisa sio kwa sehemu tu.

Kumbuka vile Yesu alivyofundisha:

> [27] Mtu ye yote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.[28] Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia? [29] Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki, [30] wakisema, Mtu huyu alianza kujenga,

akawa hana nguvu ya kumaliza.[31] Au kuna mfalme gani, akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwanza yeye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? [32] Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yuke akali mbali.[33] Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. (Luka 14:27-33)

Watu wanapaswa kuhesabu gharama kabla hawajakuwa Wakristo na natumai kuwa kijitabu hiki kitaweza kufanya wengi kugundua baadhi ya gharama hizo, lakini gharama hizo zinastahili (Warumi 8:18).

Kuna jambo la muhimu sana ambalo wengi hawatafanya na pia hakuna anayefanya kikamilifu ni:

[5] Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe;[6] Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.[7] Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche BWANA, ukajiepushe na maovu. (Mithali 3:5-7)

Hiyo siyo dhana tu ya Agano la Kale. Mtume Paulo aliandika:

[9] …tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu (2 Wakorintho 1:9)

[19] Walakini natumaini katika Bwana Yesu…[24] Nami naamini katika Bwana ya kuwa nitakuja na mimi mwenyewe hivi karibu. (Wafilipi 2:19,24)

[10] kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa kwa waaminio. (1 Timotheo 4:10)

Wengi wanaodai kuwa wa Mungu hawaamini Mungu. Hawataki

kufanya kazi kwa bidii na hata kuteswa ama kudharauliwa.

Wakristo wanapaswa kuamini Mungu na kuwa na upendo:

> [13] Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.[14:1] Ufuateni upendo (1 Wakorintho 13:13-14:1)

Wakristo wanapaswa kumpenda Mungu na jirani yake (Mathayo 22:37-40) na hiyo inahitaji kufuata njia ya imani katika maisha ya Mkristo.

**Kuijenga Tabia ya Upendo ndiyo Inayohusu Maisha Haya**

Lakini waweza kusema kwamba ninachohitaji ni kuamini. Mashetani pia wanaamini (Yakobo 2:14-20) na Yesu alisema kwamba kumtaja peke yake haitoshi:

> [21] Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.[22] Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? [23] Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; condokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. (Mathayo 7:21-23)

Wengi wamedai kuwa Wakristo, lakini wamekataa kuishi kama Wakristo. Yesu hawajui wao.

Imani ni kitu cha muhimu (kwa kujua zaidi, soma kijitabu chetu cha mtandao *Imani kwa Wale Walioitwa na Kuchaguliwa*). Pia kumbuka alichoandika Mtume Paulo:

> [1] Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,[2] ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kusimama katika tumaini la utukufu wa Mungu.[3] Wala si

> hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi;[4] na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo ni tumaini;[5] na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi. (Warumi 5:1-5)

Katika mwanzo wa karne ya 2, Ignato wa Antiokia alifundisha upendo, tabia na Kristo akiishi ndani ya maisha yetu kama Wakristo:

> …waumini wana tabia ya Mungu Baba kupitia kwa Yesu Kristo katika upendo, ambao katika yeye tusipokuwa tayari kukufa katika shauku yake, uhai wake haumo ndani mwetu. (Ignatius' Letter to the Magnesians, Chapter 5. Roberts & Donaldson, anti-Nicene Fathers).

Wakati Biblia inataja kwamba kukua kitabia ni muhimu (Warumi 5:4; Wafilipi 2:22), yafuatayo ni jinsi Herbert Armstrong alifundisha kuhusu tabia:

> Kwa hivyo sikiliza kwa makini ukweli mkubwa muhimu- tabia, takatifu na ya haki ndiyo ufanikishaji mkubwa unaoonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu Muumbaji-hiyo ndiyo pia njia mkubwa ya kusudi lake. Yaani shabaha kuu.

Lakini kwa njia gani?... tabia kamilifu lazima tuikuze. Inahitaji uhuru na uamuzi wa taasisi tofauti ambayo inafaa iundwe. Lakini, zaidi ya yote, lazima iwekwe na itoke kwa Mungu ambaye ana tabia hiyo ya haki kuitia.

> Tabia kamilifu, takatifu na ya haki ni uwezo katika taasisi mbalimbali ya kutambua njia ifaayo na isiyofaa, kusalimu kwa njia ya hiari kwa Mungu na kufuata njia yake kamilifu-kukubali kutawaliwa na Mungu-kusimama dhidi ya majaribu na ubinafsi, kuishi na kutenda mema. Na hata tabia hiyo takatifu ni karama ya Mungu. Inakuja kwa

> kukubali Mungu ili aziweke amri zake (maisha yaafayo ya Mungu) ndani ya mtu ambaye ameamua na anataka.
>
> Kwa kweli, tabia hii kamilifu yatoka kwa Mungu peke yake, na anaweka ndani ya mtu ye yote ambaye ameumba, wakati wamekubali hata baada ya mateso mengi na majaribu ya ajabu.
>
> Mungu alitufanya kwa mfano wake, kwa sura yake (umbo na muundo), tukiwa na mata bila Roho. Lakini Mungu anasema, *Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Yesu Kristo (*Wafilipi 2:5). (Armstrong HW. The Incredible Human Potential, 1978, pp. 39-40, 52).

Kwa njia nyingine, kwa sababu wale walioitwa na Mungu wanajaribu kuishi kulingana na Amri zake, watakuwa na mateso na majaribu ambayo yatajenga aina ya ''tabia'' (Warumi 5:1-4) ambayo pia ina aina ya ''ushuhuda wa dhamiri yetu'' (2 Wakorintho 1:12), ambao Mungu anataka wana wake wamiliki.

Tazama tena vile Herbert W. Amstrong alivyoandika:

> Roho ya binadamu pekee haiwezi kuona, kusikia, kufikiri ama kujua. UHAI pekee, asili na inayojumuisha, unapatikana katika Roho Mtakatifu wa Mungu, inayoungana na roho wa mwanadamu… Wakati wa kifo, ''Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa'' (Mhubiri 12:7). Roho ni mahali pa kuhifadhi kumbukumbu na tabia. Roho ni kama ukungu. Inahifadhi hata umbo la mwanadamu na mwundo wa aliyekufa, ili kwamba wakati wa kufufuka kwa hukumu wale waliokufa watafanana vile walivyokuwa awali kabla hawajafa, na pia watahifadhi ile tabia waliokuwa nayo katika maisha yao, na kukumbuka yale yote yaliyohifadhiwa kwa akili zao. Lakini wakati baada ya kifo, hakuna kumbukumbu lolote- ''wafu

hawajui chochote'' (Mhubiri 9:5).

> Tutauridhi ufalme wakati Kristo atakapokuja. Waliokufa katika Kristo watafufuliwa, wapae kwanza wakibadilishwa kuwa Roho isiyokufa… (Amrstrong HW. Mystery of Ages, 1985, pp. 110, 127, 344-345).

Twapitia mateso na majaribu katika maisha ili tuijenge tabia ya ufufuo. Mtume Paulo aliandika:

> [13] Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahizunika kama na wengine wasio na matumaini.[14] Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, viviyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.[15] Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti.[16] Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, naparapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.[17] Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.[18] Basi, farijianeni kwa maneno hayo. (1 Wathesalonike 4:13-18)

Kwa hivyo Wakristo wanaweza kuwa na maisha yasiyokuwa na maana ikiwa hakuna ufufuo. Lakini kwa sababu kuna ufufuo, tunalo tumaini la kufariji.

Polycarp wa Smirna, aliandika yafuatayo katika karne ya 2, kama vile Paulo alivyoandika kuhusu upendo, imani na tumaini:

> Mambo haya nawaandikia ndugu zangu, kuhusu haki, sio kwamba nayachukuwa kila kitu kwa njia yangu, bali ni kwa sababu mliniita nifanye hivyo. Kwa sababu hakuna

> mtu anayeweza kuifikia hekima ya baraka aliyokuwa nayo Paulo. Yeye, miongoni mwenu, alifundisha neno la kweli kikamilifu na kwa bidii miongoni mwa wale waliokuwa hai. Na alipokosa kuwa miongoni mwenu, aliandika waraka, ambayo mkiisoma kwa makini, mtapata ndiyo njia ya kuwajenga katika imani ambayo mlipewa, na ambapo mlifuata na tumaini na kuongeza na upendo kwa Mungu, na Kristo, na jirani yetu (Polycarp. Letter to the Phillipians, chapter III).

Kumbuka pia alichoandika Mtume Paulo:

> 18 Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu. (Warumi 8:18)

> 9 Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuyaingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. (1 Wakorintho 2:9)

Kwa njia nyingine, Mtume Paulo anafundisha kwamba kuishi kwa njia ya Mkristo ni zaidi ya vile unavyodhani.

Yesu aliahidi sehemu ya kipekee kwa kila Mkristo na akafundisha kwamba wote watatuzwa kulingana na kazi zao, kama vile Mtume Paulo pia:

> 2 Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. (Yohana 14:2)

> 24 Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate. 25 Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona. 26 Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, nakupata hasara ya nafsi

yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? [27] Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. (Mathayo 16:24-27)

[8]…kila mmoja atalipwa kulingana na kazi yake (1 Wakorintho 3:8 NBT).

Mtume Paulo alimwita Shetani ‘’mungu wa dunia hii’’ (2 Wakorintho 4:4) ama kwa njia ifaayo, ‘ni mungu wa ulimwengu huu.’’ Yesu alimwita Shetani, ‘’mkuu wa ulimwengu huu’’ (Yohana 12:31). Ulimwengu hauheshimu amri za Mungu, Lakini wanaenda kwa njia ya Shetani.

Wakristo wanapaswa kuishi kwa njia tofauti na ya ulimwengu.

Biblia pia inataja jinsi ya kuishi kama Mkristo kama ‘’Njia’’ (Matendo 24:14,22) ama ‘’Njia ya Bwana ‘’ (Matendo 18:25). Inapaswa pia kuitwa ‘’njia ya haki’’ (2 Petro 2:21). Petro pia aliandika:

[2] Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu (2 Petro 1:2)

[17] Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.[18] Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele. (2 Petro 3:17-18)

Maisha ya Mkristo hayabaki palepale. Tunapaswa kukua katika neema na katika maarifa. Kumbuka pia:

[14] Watu wenye akili huweka akiba ya maarifa (Mithali 10:14)

[15] Angalieni mtu awaye yote asimlipe mwenziwe mabaya kwa mabaya; bali siku zote lifuateni lilio jema, ninyi kwa

> ninyi na kwa watu wote.[16] Furahini siku zote; [17] ombeni bila kukoma; [18] shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.[19] Msimzimishe Roho; [20] msitweze unabii [21] jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema; [22] jitengeni na ubaya wa kila namna. (1 Wathesalonike 5:15-22)

> [9] Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile niliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni;[10] mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu, [11] mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha. (Wakolosai 1:9-11)

Maarifa hayo yanatoka kwa neno la Mungu na mahubiri n. K. (Warumi 10:14-17)

Mabadiliko siyo rahisi. Mara nyingi yanapingwa. Wengine wanajifanya kama kijiti cha kiroho kilichokwama matopeni. Viongozi wa kanisa la awali walijulikana kuwa na moyo mkunjufu wa kubadilika. Yesu Kristo alikuja na akaleta nuru na ukweli (Yohana 12:46; 14:26 n. K), lakini ulimwengu wa wakati huo wahalikana nuru. Hata na wale waliokuwa wakidhani ya kwamba wao ni watu wa Mungu.

> [11]Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. (Yohana 1:11)

Viongozi wa madhehebu ya wakati wa Yesu hawakukubali ukweli ulioletwa na Yesu kutoka kwa Mungu Baba.

Yesu, kwa njia nyingine ‘’aliyumbisha mashua yao.’’

Yesu alikuwa akienenda kinyume na hali yao ya kawaida au cheo chao. Na wakati ulidhani kwamba Mafarisayo na Masadukayo wangebadilika-hata hivyo wangepaswa kubadilika-basi na wewe je, Waweza kubadilika? Inasemekana kwamba ''kimasomo, Mafarisayo hawangeweza kupinga hekima aliyokuwa nayo Yesu alipokuwa akiongea'' na kwamba ''walijaribu kwa hisia zote kumpinga hata kufikia kiwango cha kumsulubisha!''

Roho na tabia hiyo ya kushikilia mapokeo yao katika maisha ya Mafarisayo wa leo zinapatikana miongoni mwa wale wanaokiri kuwa Wakristo ambao wanapinga mabadiliko.

Usiwe kama wao. Mkristo wa kweli atabadilika na kumtii Mungu:

> 7 Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. 8 Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, nakuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. 9 Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, nafuraha yenu kuwa hamu. 10 Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza. (Yakobo 4:7-10)

Wakristo wanapaswa kuwa viumbe WAPWA:

> 17 Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. (2 Wakorintho 5:17)

Kwa hivyo, maisha ya Mkristo LAZIMA yabadilike kutoka kwa yale ya awali.

Zaidi ya hayo, Wakristo wanapaswa kuijua Biblia na ukweli ambao unatutenganisha na mfumo wa ulimwengu wa Babeli wa uongo ambao Shetani ameudanganya (Ufunuo 12:9):

> [31]Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli;[32] tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. (Yohana 8:31-32)

> [16]Wao sio wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.[17] Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli. (Yohana 17:16-17)

Wakristo wameridhiwa ''upendo wa ukweli'' ili kwamba wasije kudanganya kama wengine watakavyofanya (2 Wathesalonike 2:7-14).

**Huwezi Kupata Wokovu kwa Matendo**

Wengine, hasa wale walio na msingi wa Kiprotestani wanadhani kwamba kazi wanazozifanya zinaweza kuuwapa wokovu.

Lakini si hivyo.

Hakuna mtu ye yote anayeweza kupata wokovu kwa uwezo wake mwenyewe:

> [8]Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. (Waefeso 2:8-9)

Lakini tazama mstari unaofuata:

> [10]Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo. (Waefeso 2:10)

Hata kama mtu hawezi kupata wokovu kwa uwezo wake, Wakristo wanatarajiwa kuwa na aina ya matendo ambayo Mungu anataka.

Na Wakristo wanapaswa kunyenyekea kuhusu haya yafuatayo:

> 8Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na
> BWANA anataka nini kwako, ila kutenda haki, nakupenda
> rehema, nakwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!
> (Mika 6:8)

> 1Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana,
> mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa;
> 2kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu,
> mkichukuliana katika upendo; 3na kujitahidi kuuhifadhi
> umoja wa Roho katika kifungo cha amani.4 Mwili mmoja,
> naRoho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja
> la wito wenu.5 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo
> mmoja.6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu
> ya yote na katika yote na ndani ya yote.7 Lakini kila
> mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha
> kipawa chake Kristo. (Waefeso 4:1-7)

Mfuasi wa kweli wa Mungu anafanya haki na kupenda rehema. Wakristo hawaokoki kwa matendo lakini kwa neema ya Mungu na rehema yake. Kumbuka pia:

> 3 Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,
> ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili
> tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu
> Kristo katika wafu; 4 tupate na urithi usioharibika, usio na
> uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.5
> Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani
> hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa
> mwisho. (1 Petro 1:3-5)

Mungu alituma mwana wake kupitia kwa rehema yake ili atufie kwa ajili ya dhambi zetu.

**Wakristo wa kweli Wanaelewa Kwamba Hawawezi Kuchagua Kutotii**

Mungu anatarajia kwamba watu wake wamtii:

> [1] Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe; [11] maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo. (2 Petro 1:10-11)

> [17] Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? (1 Petro 4:17)

Wengi wanaamini kwamba wanaweza kuwa Wakristo nusu.

Wanadhani kwamba bora tu wanaweza kuamini na wanafanya sehemu tu ya mapenzi ya Mungu, Basi Mungu atawaelewa.

Ni ukweli kwamba Mungu ataelewa. Ataelewa kwamba humpendi kama vile inavyotakikana. Kumbuka pia yafuatayo:

> [37] Akamwambia, mpende Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, nakwa akili zako zote.[38] Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.[39] Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.[40] Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. (Mathayo 22:37-40)

Kutotii kwa hiari kumelaaniwa katika Biblia:

> [26] Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; [27] bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, naukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.[28] Mtu

aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa
neno la mashahidi wawili au watatu.[29] Mwaonaje?
Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule
aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, nakuihesabu damu ya
agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, nakumfanyia
jeuri Roho wa neema? (Waebrania 10:26-29)

Usiwe ''Mkristo anayechagua '' ambaye anachagua amri ya Mungu ya kuitii.

Kutii nusu kumelaaniwa:

[8] Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama
ilivyoandikwa, mpende jirani yako kama nafsi yako,
mwatenda vema.[9] Bali mkiwapendelea watu, mwafanya
dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji.[10]
Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila
akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.[11] Kwa
maana yeye aliyesema, usizini, pia alisema, usiue. Basi
ijapokuwa hukuzini, Lakini umeua, umekuwa mvunja
sheria.[12] Semeni ninyi, nakutenda kama watu
watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru.[13] Maana
hukumu haina huruma kwake yeye asiyeona huruma.
Huruma hujitukuza juu ya hukumu. (Yakobo 2:8-13)

Wakristo wanajaribu kumpenda Mungu na majirani, Wanajaribu kuepukana na kutotii amri za Mungu, natena wanafahamu rehema ya Mungu. Usiwe mnafiki (Mathayo 6:5). Usiangalie jinsi unavyoweza kufikia karibu na dhambi-jaribu kuepukana hata na sura ya dhambi (1 Wathesalonike 5:22).

Hiyo haimanishi kwamba Wakristo hawatendi dhambi kama vile yafuatayo yanavyotuonyesha:

[1:8] Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya
wenyewe, Wala kweli haimo mwetu.[9] Tukiziungama

dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, nakutusafisha na udhalimu wote.[10] Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twafanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.[2:1] Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, yesu Kristo mwenye haki (1 Yohana 1:8-2:1)

Dhambi haifai kufanyiwa majadiliano. Tukitenda dhambi, twapaswa kuungama dhambi zetu kama vile tumeelezwa hapo juu.

**Wakristo Wanapaswa Kuwa Upande wa Mungu**

Inafaa Wakristo wawe katika upande wa Mungu.

Mtume Paulo alisema kwamba jinsi anavyoishi inafaa iwe mfano kwetu:

> [16] Basi, nawasihi mnifuate mimi. (1 Wakorintho 4:16)

> [17] Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi. (Wafilipi 3:17)

Mifano ya Paulo ilikuwa ni kutunza desturi za Kibibalia (Matendo 28:17), kama vile Sikukuu (1 Wakorintho 5:7-8; matendo 18:21).

Mtume Paulo aliandika kwamba watu wa Mungu wanapaswa kuvumilia:

> [9] Ndugu, msinung'unikiane, msije mkahukumiwa. Angalieni, mwamuzi amesimama mbele ya milango.[10] Ndugu, Watwaeni manabii walionena kwa jina la Bwana, Wawe mfano wa kustahimili mabaya, nawa uvumilivu.[11] Angalieni, twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa

> Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma. (Yakobo 5:9-11)

Wakristo wanapaswa kuwa vielelezo, nawakati mwingine watateseka kwa sababu ya kuwa Wakristo.

Mtume Petro aliandika:

> [19] Maana huu ndio wema hasa, mtu akivumilia huzuni
> kwa kumkumbuka Mungu, pale ateswapo isivyo haki.[20]
> Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo mema na
> kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu.[21]
> Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa
> kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo
> zake.[22] Yeye hakutenda dhambi, Wala hila haikuonekana
> kinywani mwake.[23] Yeye alipotukanwa, hakurudisha
> matukano;alipoteswa, hakuogofya; bali alijikabidhi kwake
> yeye ahukumuye kwa haki.[24] Yeye mwenyewe
> alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti,
> tukiwa wafu kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake
> mliponywa. (1 Petro 2:19-24)

Kama vile Yesu alikuwa kielelezo kwetu, nasi pia tunapaswa kuwa vielelezo kwa wengine.

> [6] Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha
> kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya
> Roho Mtakatifu.[7] Hata mkawa kielelezo kwa watu wote
> waaminio katika Makedonia, nakatika Akaya. (1
> Wathesalonike 1:6-7)

> [13] Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, Bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi

mnaoamini.[14] Maana ninyi, ndugu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu; kwa kuwa mlipata mateso yale yale kwa watu wa taifa lenu wenyewe, Waliyoyapata na hao kwa Wayahudi. (1 Wathesalonike 2:13-14)

Wafuasi wa Paulo waliokuwa kule Thesalonike walifuata mfano wa wale waliokuwa Uyahudi na wakawa mifano kwa wengine kupitia kwa mateso yao kama Wakristo.

Yesu aliwafundisha Wakristo kuwa ''nuru ya ulimwengu'' (Mathayo 5:14).

Hii inamaanisha kwamba tunaishi tofauti na ulimwengu:

[15] Msiipende dunia, Wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.[16] Maana kila kilichomo duniani, yaani, taama ya mwili, natamaa ya macho, nakiburi cha uzima, havitokani na Baba, Bali vyatokana na dunia.[17] Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, Bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu milele. (1 Yohana 2:15-17)

Na wakati wengi wanadhani kwamba hawapendi ulimwengu, Wanaelewa kwamba Mungu anatarajia watu wake wawe upande wake:

> [13] Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia, tazama, mtu mume akasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa na upanga wazi mkononi mwake; yoshua akamwendea, nakumwambia, je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu? [14] Akasema, La, Lakini nimekuja sasa, nili amiri wa jeshi la BWANA. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mtumishi wake? (Yoshua 5:13-14)

Yoshua alichaguliwa na Mungu (Hesabu 27:18), Lakini kumbuka

kwamba angeambiwa kwamba awe upande wa Mungu. Kuwa upande wa Mungu, kuishi kwa njia yake, ndiyo inafanya Mungu kuwa upande wetu.

Wakristo wanapaswa kuwa upande wa Mungu. Wakati mwingine kuwa upande wa Mungu inafanya tunakuwa na shida na madhehebu mengine.

Je! Hiyo ina maana kwamba tunaweza kulegeza?

Hapana.

Mtume Yohana aliandika:

> 21 Sikuwaandikia ninyi kwa sababu hamwijui iliyo kweli, Bali kwa sababu mwaijua, tena kwamba hapana uongo wo wote utokao katika hiyo kweli. (1 Yohana 2:21)
>
> 3 Maana nalifurahi mno walipokuja ndugu na kuishuhudia kweli yako, kama uendavyo katika kweli.4 Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli. (3 Yohana 3-4)
>
> 11 Mpenzi, usiuige ubaya, Bali uige wema. Yeye atendaye wema ni wa Mungu, Bali yeye atendaye mabaya hakumwona Mungu. (3 Yohana 11)

Hakuna uongo upatikanao kwa ukweli. Wale wasioishi kama Wakristo sio ndugu zetu wa Kiroho.

Biblia ina onyo kwa watu wa Mungu wengine katika nyakati za mwisho:

> 2 …Babeli…4 …Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, Wala msipokee mapigo yake. (Ufunuo 18:2,4)

Basi tufanyeje?

Pamoja na kutolegeza na madhehebu ya uongo wa ulimwengu huu, kumbuka kwamba Yesu alifundisha:

> [44] lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, Waombeeni wanaowaudhi. (Mathayo 5:44)

Uwe na imani (tazama kijitabu chetu kwa mtandao wa tovuti: Imani kwa Wale Walioitwa na Kuchaguliwa) ya kuishi kama Mkristo na uombe (tazama kijitabu chetu kwa mtandao wa tovuti: Maombi: Biblia Inafundisha Nini?)

Kumbuka mafungu mengine kutoka kwa Agano la Kale:

> [13] Kama baridi ya theluji wakati wa mavuno; ndivyo alivyo mjumbe mwaminifu kwao wamtumao; kwa maana huwaburudisha bwana zake nafsi zao. (Mithali 25:13)

> [17] Mjumbe mbaya huanguka maovuni; bali mjumbe mwaminifu ni afya. (Mithali 13:17)

Kumbuka pia kile ambacho Mtume Yakobo alitiwa msukumo kuandika:

> [26] Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, Wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai.[27] Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, nakujilinda na dunia pasipo mawaa. (Yakobo 1:26-27)

Kuwa na kiasi, kufanya mema, nakutolegeza kwa mambo ya ulimwengu ni yale ambayo Wakristo wa kweli wanafaa kufanya. Tunafaa tusaidie wale tunaweza kusaidia:

> [9] Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.[10] Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio. (Wagalatia 6:9-10)

Ukristo wa kweli sio wa kuangalia nafsi yako pekee.

## 4. Uwezekano Wetu ni Mkubwa kwa Sababu Mungu Yuko Upande Wetu

Biblia inafundisha:

> [31] Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? [32] Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, Bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? (Warumi 8:31-32)

Sisi ambao tuko upande wa Mungu tutashinda.

Yesu alisema:

> [12] Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa.[13] Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. (Mathayo 24:12-13).

Mtume Paulo alitiwa msukumo kuandika:

> [2] Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.[3] Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo,[4] sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, [5] kwa sababu ya ushirika wenu katika kuineza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi.[6] Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. (Wafilipi 1:2-6)

> [35] Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? [36] Kama ilivyoandikwa ya kwamba, kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa.[37] Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, nazaidi ya kushinda, kwa yeye

> aliyetupenda.[38] Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, Wala mauti, Wala uzima, Wala malaika, Wala wenye mamlaka, Wala yaliyopo, Wala yatakayokuwapo, Wala wenye uwezo, [39] wala yaliyo juu, Wala yaliyo chini, Wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. (Warumi 8:35-39)

> [12] Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.[13] Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu, atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. (1 Wakorintho 10:12-13).

Sasa, hiyo inamaanisha kwamba unaacha kufanya jambo fulani na badala yake unafanya jambo jingine. Hiyo ni mbinu ambayo inaweza kukusaidia ukukumbana na magumu na kuchanganyikiwa.

Uwezekano wako ni mkubwa:

> [5] Maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao tunaounena, ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema, [6] Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu hata umwangalie? [7] Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono yako;[8] Umeweka vitu vyote chini nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hamjaona vitu vyote kutiwa chini yake,[9] ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ila kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.[10] Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na

> kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso.[11] Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; [12] akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikakati ya kanisa nitakuimbia sifa.[13] Na tena, nitakuwa nimemtumaini yeye. Na tena Tazama mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu (Waebrania 2:5-13)

Wakristo wanapaswa kuwa watoto wa Mungu ili wapate kutawala duniani kote katika Ufalme wa Mungu!

Mungu ‘’anatafuta mzao mwenye kumcha Mungu’’ (Malaki 2:15)

> [34] Yesu akawajibu, je! Haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba, mimi nimesema, ndinyi miungu? [35] Ikiwa aliwaita miungu wale waliojiliwa na neno la Mungu; (na maandiko hayawezi kutanguka);[36] je! Yeye ambaye Baba alimtakasa, akamtuma ulimwenguni, ninyi mnamwambia, unakufuru; kwa sababu nalisema, mimi ni Mwana wa Mungu? (Yohana 10:34-36)

Paulo aliandika kwamba Yesu ni mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi:

> [29] Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. (Warumi 8:29)

Kumbuka kwamba kuna ndugu wengi.

Kumbuka kwamba kile kilichofanyika kwa Yesu Kristo, kitatupata pia:

> [20] Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, Limbuko lao waliolala.[21] Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu,

> kadhalika na kiyama ya watu ililetwa na mtu.[22] Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.[23] Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja. (1 Wakorintho 15:20-23)

> [18] Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake (Yakobo 1:18).

> [4] Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake, kwa maana ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa wamenunuliwa katika wanadamu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. (Ufunuo 14:4)

> [16] Tena malimbuko yakiwa matakatifu, kadhalika na donge lote; na shina likiwa takatifu, matawi nayo kadhalika (Warumi 11:16).

Wakristo wanapaswa kuwa malimbuko ya kwanza kama Kristo. Kama malimbuko ya kwanza, kristo ni mtakatifu.

Kumbuka jinsi Yesu alivyoomba:

> [10] na wote walio wangu ni wako, nawalio wako ni wangu; nami nimetukuzwa ndani yao.[11] Wala mimi simo tena ulimwenguni, Lakini hawa wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba mtakatifu kwa jina lako ulilonipa, uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo. (Yohana 17:10-11)

Kwa vile Mungu Baba na Mwana ni watakatifu, yesu aliwaombea wafuasi wake wawe na umoja kama vile yeye na Baba yake walivyo-ambayo inamaanisha kwamba wamo pamoja katika familia ya Mungu. Ila tu kama mtu anataka kufasili andiko hili tofauti, Lakini Yesu aliendelea mbele na maombi na akaomba yafuatayo:

> [20] Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoamini kwa sababu ya neno lao.[21] Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yako;hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.[22] Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja.[23] Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.[24] Baba hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo, Wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu.[26] Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua; lakini mimi nalikujua, nahao wamejua ya kuwa ndiwe uliyenituma.[26] Nami naliwajulisha jina lako, tena nitawajulisha hilo; ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao. (Yohana 17:20-26)

Yesu aliomba kwamba wafuasi wake wawe na umoja jinsi yeye na Baba wana umoja. Na wamo katika familia takatifu.

Zaidi ya hayo, kumbuka kwamba Biblia inafundisha kwamba kuna familia nzima inayoitwa kwa jina la Mungu Baba, nakwamba tunapaswa kujua upendo wa Kristo ili kwamba tuwe na ukamilifu wa Mungu:

> [14] Kwa hiyo nampigia **Baba magoti**,[15] **ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa,**[16] awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.[17] Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani **mkiwa na shina na msingi katika upendo**; [18] ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, naurefu, nakimo, nakina; [19] **na kuujua upendo wake Kristo**, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi,

m**pate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu**. (Waefeso 3:14-19)

Ikiwa mtu amejazwa na ''utimilifu wote wa Mungu'' haimaanishi kwamba watakuwa pia kama Mungu wakiwa sehemu ya Familia ya Mungu?

Mtume Yohana alifundisha:

> 12 Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waaminio jina lake (Yohana 1:12)

> 1 Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu, nandivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye.2 Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu (1 Yohana 3:1-2a).

Watoto wa wanadamu ni wanadamu, Watoto wa ng'ombe ni ng'ombe. Je! Watoto wa Mungu wataitwaje?

Mtume Petro alifundisha kuhusu kupokea tabia ya Uungu:

> 3 Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.4 Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, i**li kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu**, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. (2 Petro 1:3-4)

Je! Wale walio ''waliopata ushirika wa tabia ya Uungu'' wamefanywa kama Mungu? Na kupata tabia kamili kama hii haifanyiki hadi ufufuo wa wafu (1 Wakorintho 15:50-53).

Kile ambacho Mungu ametupangia ni cha ajabu mno:

> [9] lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.[10] Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. (1 Wakorintho 2:9-10)

Ni cha ajabu sana kwamba mambo hayo wanadamu hawajawahi kuona ama kusikia.

## 5. Wakristo Wanakutana na Kuendeleza Ufalme wa Mungu

Wanafunzi wa Yesu walifundisha Ufalme wa Mungu:

> [1] Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi.[2] Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, nakupoza wagonjwa. (Luka 9:1-2)

Mtume Paulo aliandika kuhusu Ufalme wa Mungu na pia juu ya Yesu:

> [8] Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, nakuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu. (Matendo 19:8)

> [25] Na sasa, tazameni, mimi najua ya kuwa ninyi nyote niliowahubiria ufalme wa Mungu, nikienda huku na huko, hamtaniona uso tena. (Matendo 20:25)

> [23] Wakiisha kuagana naye siku, Wakamjia katika nyumba aliyokaa, Watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu…[31] **akihubiri habari za ufalme wa Mungu, nakuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo** kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu. (Matendo 28:23,31)

Kumbuka kwamba ufalme wa Mungu si juu ya Yesu Kristo (ijapokuwa yeye ndiye sehemu kubwa ya Ufalme), kwa sababu Paulo amefundisha kuhusu Yesu tofauti na vile amefundisha ufalme wa Mungu.

Paulo pia alitaja habari hiyo kama injili ya Mungu, Lakini bado ilikuwa injili ya Ufalme wa Mungu:

> [9] …tukawahubiri hivi Injili ya Mungu…[12] ili, mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita

ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake. (1 Wathesalonike 2:9,12)

Paulo pia aliita injili ya Kristo (Warumi 1:16).''Habari njema'' ya Yesu, ujumbe ambao alifundisha.

Kumbuka kwamba haikuwa tu injili kuhusu nafsi ya Yesu Kristo ama kuhusu wokovu wa mtu binafsi. Paulo alisema kwamba injili ya Yesu Kristo ni pamoja na kumtii Yesu, kurudi kwake, nahukumu ya Mungu:

> [6] ... Kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi;[7] na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake [8] katika mwali wa moto;huku akiwapiliza kisasi wao wasiomjua Mungu, nawao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu;[9] watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; [10] yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, nakustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, (kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu). (2 Wathesalonike 1:6-10)

Mabalozi wa Ufalme wa Mungu wanashiriki katika kutekeleza ujumbe wa kuhubiri.

**Wakristo Wanafiladelfia Wanapenda Wengine, ni Waaminifu kwa Mafundisho, naWanapitia Milango iliyowazi**

Biblia inaonyesha kwamba kuna aina tofauti ya Wakristo katika siku za mwisho (Ufunuo 3). Yesu alisema yafuatayo kwa Wakristo Wanafiladelfia:

> [7] Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye.[8] Nayajua matendo yako. Tazama, nakupa mlango

> uliofunguliwa mbele yako mbele yako, ambao hakuna awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza neno langu, Wala hukulikana jina langu.[9] Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, Wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, Bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, nakujua ya kuwa nimekupenda.[10] Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujiliwa ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi.[11] Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.[12] Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, Wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, najina la mji wa Mungu wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu wangu, najina langu mwenyewe, Lile jipya.[13] Yeye aliye na sikio, naalisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. (Ufunuo 3:7-13)

Filadelfia inamaanisha ‘’upendo wa ndugu’’ ama ‘’kuwa na uzoefu kwa ndugu.’’ Wanafiladelfia wanaonyesha upendo huo kwa kuonyesha uhusiano wa kutosha kuhusu wengine ili wafanye kazi na kutimiza kuhubiri na maandiko mengine.

Yesu alisema:

> [14] Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote;hapo ndipo ule mwisho utakapokuja. (Mathayo 24:14)

Yesu aliwapa Wanafiladelfia mlango ulio wazi-hiyo inamaanisha kwamba ni mlango wa kuutangaza injili (2 Wakorintho 2:12;1 Wakorintho 16:8-9; Wakolosai 4:2-4). Kuitangaza injili, kufanya kazi ya kuitimiza Mathayo 24:14, nakuwa mwaminifu ni tabia zote za Wakristo Wanafiladelfia.

Mathayo 24:14 LAZIMA INAREJELEA Wakristo WANAFILADELFIA kwa sababu Mungu ameisifu kazi ya Wanafiladelfia, hata hivyo amekemea kazi za Walaodekia, ambao ndio Wakristo wengi wanaopatikana sasa kabla ya Dhiki Kuu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba Wakristo wengi katika nyakati za mwisho hawana haja ya kuwa mabalozi wa sehemu ya Kanisa la Mungu la Kifiladelfia.

**Wapendwa Waliotawanyika**

Katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), tuna wapendwa wanaopatikana kote Marekani na Kanada na hata Karibiani (kama vile Trinidadi na Tobago), asia, afrika, marekani Kusini, nasehemu nyingine. Tuna washirika katika bara zote za dunia ambazo watu wanamiliki na hasa wengi katika Marekani.

Lakini kwa sehemu nyingi nje ya Afrika, hatuna kusanyiko karibu (ukitaka kutazama makusanyiko yetu basi tazama www.ccog. Org).

Katika nyakati zijazo, tunatarajia kuwa na makusanyiko mengi katika maeneo mengi, kwa sababu tunapata kuongezeka kila mwaka. Kwa hivyo, ikiwa hakuna kusanyiko karibu nawe, usipoteze tumaini-subiri tu, kwa uaminifu, napengine kwa wakati ufaao, tutakuwa na kundi/kusanyiko karibu nawe. Labda litakuwa lile ambalo umesaidia kuliunda!

Yesu alifundisha kwamba, ''wengi wameitwa na wachache wamechaguliwa'' (Mathayo 22:14). Mmoja wa wale ambao wanapoteza tumaini kwa sababu hakuna kundi karibu nawe.

Biblia inafundisha:

> 4 Nawe utajifurahisha kwa BWANA, naye atakupa haja za moyo wako.
> 5 Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya.
> 6 Ataitokeza haki yako kama nuru, nahukumu yako kama adhuhuri.
> 7 Ukae kimya

> mbele za BWANA, nawe umngojee kama saburi; usimkasirikie yeye afanikiwaye katika njia yake, Wala mtu afanyaye hila. (Zaburi 37:4-7)

Wakati mwingine Wakristo wanapaswa kusubiri na kuamini Mungu ili asimamishe makundi karibu nao.

Kumbuka, yesu aliahidi Wakristo Wanafiladelfia kwamba watakuwa ‘’nguzo’’ katika Hekalu la Mungu (Ufunuo 3:12). Kwa hivyo katika kipindi hiki, Wakati mwingine kuwa katika sehemu ya msingi ya kundi jipya, nahata kusimama katika sehemu peke yako, huenda ikawa ni sehemu ya kujifunza ili upate ujira.

Bila shaka, tunapaswa kukusanyika kila Sabato ikiwezekana (Waebrania 10:24-25). Sikukuu za Mungu kama Makambi, ni nafasi nzuri kukusanyika (Walawi 23:2; warumi 12:1).

Katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), tunakuwa na Sikukuu ya Makambi katika maeneo mengi kote ulimwenguni. Sikukuu hii ni wakati ambapo Mungu anatarajia wale wanaoweza kusafiri (Zaburi 42:4); mbali ikiwezekana (Kumbukumbu 14:22-27). Sikukuu hii pia inawapa Wakristo Wanafiladelfia nafasi ya kushiriki pamoja.

Katika karne ya 20, hasa katika siku za awali ya Redio Kanisa la Mungu, Watu mara nyingi wangesubiri miaka mingi kupata fursa kusikia mahubiri ama kupata njia ya mawasiliano ya Wakristo ambao wana mawazo yanayofanana. Ili kuhudumia wapendwa waliotawanyika katika karne hii ya 21, tunaandika baruapepe ya kila wiki iitwayo Barua ya Wapendwa. Ina pendekezo la ratiba ya Sabato, napia, ikiwezekana, habari ya Sikukuu. Kwa hivyo, mahubiri ya kila mara yapo kwa wale wanaotaka.

Zaidi ya hayo, Barua ya kila wiki ina habari za mambo yanayoendelea mbele katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) kote ulimwenguni. Ukiwa unataka kupokea barua hii, Basi wasiliana na Dr. Bob Thiel, kwa baruapepe cogwriter@aol.com

Omba na kuwa na subira na uamini Mungu (Mithali 3:5-7) kwamba atawaita watu ambao mtashiriki nao.

Kama nguzo, unaweza kuwa balozi wa Ukristo wa Kifiladelfia.

**Wakristo Wanaishi Kwenye Njia ya Mungu**

Wakristo wanaishi kwenye njia ya Mungu ya uzima katika dunia hii. Tunapaswa kuishi kama mabalozi wa Ufalme wa Mungu.

Maelezo mengine ambayo kijitabu hiki kilipitia kinaonekana magumu, nandiyo yanawezakuwa magumu wakati mwingine. Na hivyo kuna mengine ambayo yangeongezwa, Lakini natumai kwamba maelezo ya jumla yatasaidia wale watakaosoma.

Wakati Mungu ana sheria na amri ambazo zinaleta mema kwetu, elewa kwamba njia zake zinahusu upendo. Upendo kwetu sisi na upendo kwa wengine.

Ukweli ni kwamba Wakristo wanapaswa kuishi kwa njia tofauti na jinsi ulimwengu unavyoishi. Hii inawasaidia wawe na tabia ambazo watatumia baadaye katika Ufalme. Wakristo watapewa ujira kulingana na kazi zao (Mathayo 16:27; 1 Wakorintho 3:8).

Wakristo watatawala na Yesu:

> [9] …ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa,[10] ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao watamiliki juu ya nchi. (Ufunuo 5:9-10)
>
> [6] Heri, namtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja nao hiyo miaka elfu. (Ufunuo 20:6)
>
> [4] nao watamwona uso wake, najina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.[5] Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa

> Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. (Ufunuo 22:4-5)

Na habari njema ni kwamba Yesu atarudi na atauanzisha wakati ambao utatimiliza matokeo hayo yalioonenwa:

> 3 Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.
> 4 Naye atafuta kila chozi katika macho yao, Wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, Wala kilio, Wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. (Ufunuo 21:3-4)

Na hiyo ni sehemu ya habari njema ya kuwa Mkristo ukitawala na Yesu katika Ufalme.

Je! Utaishi maisha haya?

Kuishi kama Mkristo, unaishi kama balozi wa Ufalme wa Mungu unaokuja.

# Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG)

Afisi ya Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG) inapatikana :1036 W. Grand Avenue, Grover Beach, California, 93433 USA. Tuna washirika kote ulimwenguni, nabara zote zinazomilikiwa na watu (bara zote, ila tu Antaktika).

### Taarifa za Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG) kwenye Tovuti

**CCOG. ORG** Tovuti ya kamili ya Kanisa la Mungu Linaloendelea.

**CCOG. ASIA** Tovuti inayolenga Asia na lugha nyingi za Kiasia.

**CCOG. IN** Tovuti inayolenga India, ambayo ina lugha tofauti ya Kihindi.

**CCOG.EU** Tovuti inayolenga Ulaya, ambayo ina lugha tofauti za Ulaya.

**CCOGAFRICA**. O**RG** Tovuti inayolenga Afrika.

**CCOGCANADA**.**CA** Tovuti inayolenga Kanada

**CDLIDD.ES** Tovuti inayolenga hasa lugha ya Kihispania.

**PNIND. PH** Tovuti inayolenga Wafilipino na ina lugha ya Kitagalogi.

# Redio na Chaneli za Video vya YouTube

**BIBLENEWSPROPHECY. NET** Redio ya mtandao ya Unabii wa Habari za Biblia.

**Bible News Prophecy Channel**. Mafundisho ya YouTube .

**CCOGArica channe**l. Ujumbe wa YouTube video kutoka Afrika.

**CCOG Animations** Picha za video vya YouTube.

**CDLIDDSermons channel**. Ujumbe wa YouTube katika lugha ya Kihispania.

**ContinuingCOG Channel**. Mahubiri ya YouTube.

# Habari na Tovuti za Historia

**CHURCHHISTORYBOOK.COM** Tovuti ya historia ya Kanisa.

**COGWRITER.COM** Tovuti ya habari, historia na unabii.

# WAKRISTO:MABALOZI WA UFALME WA MUNGU

Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma…Maana ninyi ndugu,mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi katika Kristo Yesu
(1 Wathesalonike 2:13-14)

Upendano wa ndugu na udumu.
(Waebrania 13:1)

Ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.
(Yuda 3)

Je! Wakristo wa awali waliishije?
Je! Wakristo wa sasa wanapaswa kuishi namna gani?
Je! Wajua kuiga kanisa la awali la Mungu ambalo lilikuwa Yerusalemu/Uyahudi?
Je! Wajua kujitahidi kuishi kama mjumbe wa Ufalme wa Mungu?
Hiki kijitabu cha Kibiblia kinajaribu kuyajibu maswali na mengi!



Picha inaonyesha baadhi ya matofali chache yaliyobaki (pamoja na baadhi yaliyoongezwa baadaye) ya jengo katika Yerusalemu ambalo wakati mwingine linaitwa Nyumba ya mapumziko,lakini baadaye likaitwa Kanisa la Mungu linalopatikana kwenye mlima wa Magharibi mwa Yerusalemu (ambalo siku hizi huitwa Mlima Sayuni).Inaaminika kwamba ndiyo eneo la jengo la Kanisa la Wakristo wa awali.Matofali kutoka hekalu ya Wayahudi yaliyoharibiwa na Warumi mwaka 70 B.K yanaaminiwa ya kwamba yalitumika kujenga msingi na kuta za jengo hili.

Je! Unaishi kama vile waumini wa awali walivyoishi?

Je! Ungependa kujua zaidi juu ya kuishi maisha ya Kibiblia na mtazamo wa Ukristo?

Je! Wakristo walio na Imani wanapaswa kuishije katika karne ya 21?